

**HOTUBA YA KATIBU TAWALA MKOA NDUGU SMYTHIES E. PANGISA ALIYOITOA WAKATI WA MAKABIDHIANO YA VYUMBA 5 VYA UPASUAJI NA VIFAA VYA KUFANYIA UPASUAJI KATIKA KIJIKI CHA MWIMBI WILAYA KALAMBO TAREHE 19 JUNI, 2014.**

Mheshimiwa Mgeni rasmi Iddi Hassani Kimanta (Mwakilishi wa Naibu Waziri wa Afya)

Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Benjamin William Mkapu HIV/AIDS, Meja Jenerali (Mst) Herman Lupogo

Wenyeviti na Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Rukwa

Afisa Mtendaji Mkuu wa BMAF,

Wataalamu na Watendaji wa Serikali na wa BMAF

Wageni waalikwa,

Ndugu Waandishi wa Habari

**Mabibi na Mabwana,**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana mahali hapa kwa shughuli hii muhimu ya makabidhiano ya vyumba vitano (5) vya upasuaji pamoja na vifaa vya upasuaji.

Pia napenda kuchukua fursa hii kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kuwajaalia Wadau wetu wa Maendeleo Viongozi na Watendaji wa BMAF kuweza kusafiri salama na kuweza kushiriki katika tukio muhimu la leo.

Aidha kwa namna ya pekee napenda kutoa salaamu nyingi za Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya (Mb) Mkuu wa Mkoa wa Rukwa kwa Wafadhili wetu BMAF. Nimeweza kuwasiliana naye anawasalimu sana na alipenda awepo yeye binafsi lakini kutokana na ufinyu wa muda na kukabiliwa na safari muhimu nje ya nchi kwa shughuli za Serikali ameshindwa kuungana nasi

Kwa niaba ya Wananchi na Viongozi wa Mkoa wa Rukwa napenda kutumia fursa hii, kushukuru kwa kukabidhiwa vyumba (5) vya upasuaji pamoja na vifaa vyake. Mchango huo katika sekta ya Afya ni muhimu na umekuwa wakati muafaka katika mapambano dhidi ya vifo vya Mama wajawazito.

Sisi Wananchi wa Mkoa wa Rukwa tutauenzi msaada huu, kwa kuvitunza vyumba hivyo (5) pamoja na vifaa vyake pia tutatumia huduma hizo, kwa kuhamasishana kutumia vituo vyetu vya Afya pamoja na huduma zake.

Mkoa wa Rukwa leo tumepokea vyumba (5) vya upasuaji na vifaa vyake kwa mchanganuo wa (Wilaya ya Kalambo vyumba 2, Wilaya ya Nkasi vyumba 2, na Wilaya ya Sumbawanga chumba 1.)

Kwa namna ya pekee napenda kuushukuru Uongozi na Menejimenti ya Taasisi ya Benjamin Mkapa kwa kuendelea

kutusaidia katika Sekta ya Afya, maendeleo ya Sekta ya Afya katika Mkoa wa Rukwa kwa sehemu pia inatokana na mchango wa taasisi ya BMAF.

Kama ambavyo imesomwa katika taarifa ya Mtendaji Mkuu wa BMAF, ni kweli Mkoa umenufaika na juhudi za BMAF kwa kuajiri na kuleta watumishi wa afya 50 katika mkoa wa Rukwa ambao wamekuwa wanatoa huduma za tiba katika maabara ya Hospitali ya mkoa, katika hospitali za wilaya na vituo vya afya vya serikali. Mkoa umepokea Walimu tisa (9) ambao wapo katika Vyuo vilivyopo katika mkoa wetu

Kama Mkoa tumenufaika na "scholarship" kwa wanafunzi 11 kutoka wilaya ya Nkasi, Sumbawanga DC na Sumbawanga Manispaa Wanafunzi hao wapo katika Vyuo vya afya ili kupata Cheti cha Uuguzi na Afisa Tabibu Msaidizi. Taasisi ya BMAF ilikabidhi nyumba za wafanyakazi 20 kati ya 40 zinazojengwa katika Mkoa wetu mwaka 2013.

Tumeendelea kunufaika kutokana na mafunzo mbalimbali kwa upande wa menejimenti ya idara ya afya na watumishi wa afya wa vituo vya tiba, kuhusiana na utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa ukimwi, pamoja na huduma za wajawazito.

Mkoa unatambua jitihada za BMAF kwa kuimarisha sekta ya afya ndani ya Mkoa tunapenda kuwashukuru Wadau wote wa maendeleo ambao kwa namna moja au nyingine wamewezesha haya kufanyika ndani ya Mkoa, kupitia michango yao ambayo tija

yake inaonekana kwa kupunguza vifo vya Mama Wajawazito ili kufikia malengo ya Millenia ya asilimia 75 ifikapo 2015

Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Rukwa napenda kuwaomba BMAF muendelee kuelekeza nguvu zanu kwetu katika kutukwamua katika jitihada ambazo Serikali tunazifanya katika kuimarisha sekta ya Afya katika Mkoa wetu. Ili kuimarisha Sekta ya Afya ni wazi Sekta ya Umma na Sekta binafsi zinatakiwa kufanya kazi kwa pamoja. Hivyo naomba tuendeleo kufanya kazi pamoja.

Aidha kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Rukwa napenda kutuma salamu nyingi sana kwa Mzee wetu Rais Mstahafu wa awamu ya 3 Benjamin William Mkapa kwa kuanzisha Taasisi hii ya BMAF imetufaa sana Wananchi wa Mkoa wa Rukwa.

Napenda kuwashukuru Wananchi wa Mwimbi kwa kujitokeza kwa wingi katika shughuli hii ya makabidhiano, pia nashukuru Vikundi vyote vya burudani kwa kutumbuiza na kutoa ujumbe wenye kujenga na kutia hamasa.

Asanteni sana kwa kunisikiliza

Smythies E. Pangisa  
**KATIBU TAWALA MKOA**  
**RUKWA**